--KIZIDUO--

**MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA MANEJIMENTI KILICHOFANYIKA TAREHE 2/1/2021 KATIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA KIGOMA-MAHEMBE**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

1. Bw. Achard Bajumuzi - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) - Mwenyekiti
2. Bw. Bennet Ninalwo - Kaimu Afisa Utumishi (W) - Katibu
3. Bi. Minza Edward - Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
4. Bw. Ramadhani Mpasiwakomu - Kny-Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W)
5. Bw. Chrispin Misuo - Kaimu Afisa Manunuzi (W)
6. Bw. Haruna Mwikongi - Mweka Hazina (W)
7. Dr. Lusajo R. Mwakajoka - Mganga Mkuu (W)
8. Bi. Petronila P. Gwakila - Afisa Usafi na Mazingira (W)
9. Bi. Zawadi Mzelela - Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W)
10. Bw. Kaboza Malembeka - Kaimu Muhandisi wa Ujenzi (W)
11. Bi. Huruma Eugen - Kaimu Afisa Mipango (W)
12. Bw. Exavery N. Ndalikenye - Afisa Elimu Sekondari (W)
13. Bw. Adamnoor Jama - Mkaguzi wa Ndani (W)
14. Bw. George Onyango - Kaimu Mwanasheria (W)
15. Bw. Damson Sunzu - Kaimu Afisa TEHAMA (W)
16. Bi. Emmy Chiwangu - Kny Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
17. Bw. William Kafugugu - kny Afisa Elimu Sekondari (W)
18. Bw. Vicent Mhezi - Afisa Nyuki (W
19. Bi. Vumilia J. Bidya - CC

**MUHT NA. 06/18/10/2021 AGENDA NA 1. KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao, ambaye alisalimia na kuwakaribisha wajumbe kwenye kikao, alisema kuwa tunafanya kikao cha Menejimenti cha kupitia taarifa za utekelezaji za kila idara pamoja na mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti. Baada ya kusema hayo alifungua kikao saa 4:11asubuhi.

**MUHT NA 07/18/10/2021 AGENDA NA 2. KUTHIBITISHA AGENDA**

Agenda zilisomwa na kuthibitishwa na wajumbe wote kama ifuatavyo:

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 30/12/2021.
4. Yatokanayo na kikao kilichofanyika tarehe 30/12/2021.
5. Taarifa ya utekelezaji ya fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa ya Sekondari na Msingi kwa fedha za UVIKO-19.
6. Mengineyo.
7. Kufunga kikao.



Scanned with CamScanner

**MUHT NA 10/18/10/2021 AGENDA NA 5. TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA FEDHA ZA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA YA SEKONDARI NA MSINGI KWA FEDHA ZA UVIKO-19**

Mwasilishaji aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri ilimepokea jumla ya shilingi 1,500,000,000/= kutoka Serikali Kuu (fedha za UVIKO-19) kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, shule ya Sekondari shilingi 1,380,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 69 na shilingi 120,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Shule 6 shikizi za Msingi.

Alisema fedha hizo zilitumika kwa ujenzi huo na jumla ya madarasa 69 ya shule za sekondari yamejengwa na madarasa 6 ua shule za msingi yamejengwa, hivyo Halmashauri imejenga na kukamilisha maradasa 75 ya msingi na sekondari.

Mjumbe alitoa pongezi kwa timu iliyoundwa kwani imefuatilia ujenzi huo vyema na hatimaye ujenzi umekamilika kwa wakati, pia alitaka kujua kama kuna changamoto yoyote ambayo Timu iliyoundwa ilikutana nayo isemwe ili iweze kutatuliwa na wakati wa ujenzi wa madarasa mengine wajue jinsi ya kuziepuka.

Mtaalamu alisema changamoto walizokutana nazo ni zakawaida tu kulingana na hali yetu ya Halmashauri ilivyo lakini wanashukuru Halmashauri imewawezesha na kazi imekamilika kwa wakati.

Mjumbe alitaka kujua kama kuna bakaa iliyobaki na itatumika kwa matumizi gani.

Mtaalamu alifafanua kuwa ni kweli kuna kiasi cha bakaa kilichobaki na hawajajua bakaa hiyo itatumika kwa matumizi gani lakini wanasubiri maelekezo.

**MUHT NA. 12/18/10/2021 AGENDA NA 6. KUFUNGA KIKAO**

Katibu alishukuru kikao kimeanza na kumalizika salama, alisema yote yaliyoagizwa yafanyiwe kazi kisha alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao, Mwenyekiti alisema anashukuru kikao kimeanza na kumalizika salama, alisema maagizo yote yaliyotolewa yafanyiwe kazi, fedha za miradi zisimamiwe upasavyo na ikamilike kwa wakati. Alisema changamoto yoyote ya shughuli za Halmashauri inakayojitokeze aelezwe haraka ili aone jinsi ya kuitatua ili shughuli za Halmashauri ziwe zinafanyika vyema na kwa wakati. Baadaya kusema hayo alifunga kikao saa 8:11 mchana.



Scanned with CamScanner

UMETHIBITISHWA NA:

.....................
KATIBU

.....................
MWENYEKITI

18/1/202...........
TAREHE



Scanned with CamScanner

## HALMASHAURI YA WILAYA KIGOMA

## HALMASHAURI YA WILAYA KIGOMA

### IDARA YA ELIMU MSINGI

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UVIKO=19 UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA KATIKA VITUO SHIKIZI

| Na | MKOA | HALMASHAURI | JINA LA SHULE/ KITUO | TAREHE YA KUPOKEA FEDHA | FEDHA POKELEWA | FEDHA TUMIKA | FEDHA BAKAA | ASILIMIA YA UTEKELEZAJI | CHANGAMOTO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kigoma | Kigoma | Kituo shikizi Buhagara | 21/10/2021 | 40,000,000.00 | 38,711,824.00 | 1,288,176.00 | Madarasa yamekamilika kwa asilimia mia moja | Mazingra magumu, pia tgharama za usafirishaji wa vifaa ni kubwa kutoka eneo la manunuzi |
| | | | | | **40,000,000.00** | | | | |
| | | | | | | | | | |
| 2 | Kigoma | Kigoma | Kituo shikizi Rusolo | 21/10/2021 | 40,000,000.00 | 39,770,324.00 | 229,676.00 | Madarasa yamekamilika kwa asilimia mia moja | Mazingira magumu ni milimani hakuna miundmbinu ya barabara, pia ni mwambao wa ziwa Tanganyika |
| | **JUMLA NDOGO** | | | | **40,000,000.00** | | | | |

Scanned with CamScanner

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3 | Kigoma | Kigoma | Kituo shikizi Magamba | 21/10/2021 | 40,000,000.00 | 39,327,824.00 | 672,176.00 | Madarasa yamekamilika kwa asilimia mia moja | Mazingira magumu ni milimani hakuna miundombinu ya barabara ili kusafirisha vifaa, kila kifaa kinasafirishwa kwa kichwa zaidi ya kilomita saba mpaka eneo la ujenzi |
| | **JUMLA NDOGO** | | | | **40,000,000.00** | | | | |
| | **JUMLA KUU** | | | | **120,000,000.00** | **117,809,972.00** | **2,190,028.00** | | |

Scanned with CamScanner